**Tafakari la  Kibiblia: "Usikate tamaa kamwe!"**



Mumoja wa wahusika wangu wa kibiblia ninaowapenda sana ni Yusufu, ambaye hadisi yake inasimuliwa katika Mwanzo 37-50. Baba yake, Israeli, alimpenda kuliko ndugu zake wengine 11, lakini katika sehemu kubwa ya maisha yake aliteseka kwa njiya isiyo haki. Ndugu zake walimtupa ndani ya shimo na kumuuza utumwani. Alichukuliwa kwa kinguvu kutoka katika inchi ya Kanaani hadi Misri, ambako mke wa bwana wake mpya alimshitaki kwa uwongo naye akatupwa gerezani. Lakini Mungu alimlinda katika majaribu yake yote. Hatimaye, aliweza kutumia kipawa chake cha kufasiri ndoto ili kupata kibali cha Farao, mtawala wa Misri. Kutoka wakati huu usiotarajiwa, wa miujiza katika maisha yake, alipanda hadi wa pili katika uongosi, na Mungu alimtumia kuokoa watu wengi kutokana na njaa wakati wa njaa ya miaka saba.

Wakati ndugu za Yosefu walikuja kutoka Kanaani hadi Misri kutafuta chakula, waliogopa kwamba atalipiza kisasi juu yao. Hata hivyo, badala ya kuwa na uchungu, chuki, ao kulipiza kisasi, Yosefu aliamuwa kufafanua jinsi alivyotendewa isivyo haki na kikatili kupitiya macho ya imani. Kauli yake inayojulikana sasa imerudiwa mara nyingi na waamini tangu wakati huo: "Mlikusudia kunizuru," aliwaeleza ndugu zake, "lakini Mungu alikusudiya kuwa jema ili kutimiza yale yanayofanyika sasa, kuokoa maisha ya watu wengi" (Mwanzo 50:20, NIV).

Ninajuwa kwamba wengi wenu mnateseka isivyo haki kama Yusufu alivyoteseka. Kuishi Mashariki mwa Kongo ao mahali pengine pagumu sana kunaweza kuhisi kama gereza ao mbaya zaidi wakati mwingine. Wakati wako ujao haujulikani, na huenda maisha yako yakawa mikononi mwa watu wasiotegemeka ao hata wajeuri. Lakini kile unachopitia hakielezi hadithi nzima ya mapenzi na mpango wa Mungu kwa maisha yako.

Nilipokuwa nikifundisha, nikihubiri, na kufanya huduma miongoni mwa wakimbizi magaribi mwa Thailand hivi wakati ulio pita, nilivutiwa na jinsi waamini huko wanaishi

kwa imani yao. Wanaenda shule, kuwahudumiya wengine, kuhubiri Injili, kutowa huduma za matibabu, kufanya uchangishaji feza kwa ajili ya wa IDPs(Wakimbizi ndani ya inchi yao), kufundisha watoto, kutembelea na kutunza wazee, na kufanya mambo mengine mengi mazuri piya. Wanakataa kuishi kana kwamba maisha yao yamekwisha. Na ni tofauti iliyoje wanayoleta kwa watu wao na wao wenyewe!

Kwa hivyo, endelea kuweka tumaini lako kwa Mungu. Usiache kamwe kuamini kwamba Mungu anaweza kukutengenezeya fursa katika maeneo yasiyowezekana na hali mbaya zaidi. Huenda usiweze kuelewa uzowefu wako kila mara ao kuona jinsi Mungu anavyofanya kazi kwa sasa, lakini usikate tamaa ao kuacha kuamini kwamba Mungu atafanya jambo lililo njema kupitiya wewe.

Umechaguliwa na Mungu kutimiza makusudi yake mema. Maisha yako niya muhimu. Amini na uishi hili.

Pamoja na upendo wa Jesu Christo,

Dr. Tim

“Tusichoke katika kutenda mema, maana tutavuna kwa wakati wake tusipozimia roho”
(Gal. 6:9, NIV).

Timothy C. Geoffrion ni mchungaji wa zamani ambaye amekuwa akiongoza Faith, Hope, and Love Global Ministries (www.fhlglobal.org) kwa miaka 17. Anawafundisha wanafunzi wa seminari, wachungaji, na wahudumu wengine jinsi ya kujuwa, kumpenda, na kumtumikia Mungu kwa ufanisi zaidi kama viongozi wanaoongozwa na Roho katika Kongo na Kusini-mashariki mwa Asia.

Picha: Ugawanyaji wa mchele katika Kambi ya Wakimbizi ya Tham Hin kwenye mpaka wa Myanmar-Thai.